Jina…… **Nambari yako.....……**

Shule…… **Sahihi.....……**

Tarehe.....……

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI 2
JULAI/Agosti 2010
SAA 2 ½

MITIHANI YA UTATHMINI WA PAMOJA, WILAYA YA KWANZA- 2010

Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari Kenya (K.C.S.E.)

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI 2
JULAI/Agosti 2010
SAA 2 ½

Jibu maswali yote. Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

Kwa Matumizi ya Mtahini

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyooachwa.

UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafutayo kisha ujibu maswali

Maoni yetu juu ya uhuru tuliotwaa yanahitilafiana sana. Wao katika upande mmoja watu wanaofikiri kuwa kupewa uhuru ni kushikishwa upembo na kuambiwa: Haya jamaa oneni mitunda, pembeni mitunda mle mkasaze katika upande mwingine kuna wale wanaouona uhuru kama hali ya mtu kujihisi ana hiari na mamlaka ya juu ya jambo lolote lipasalo kutenda kwa mujibu wa maendeleo yake mwenyewe na ya jamaa kwa jumla. Kundi la tatu ni la wale wasiojua maana ya uhuru wao hukiri na kuitikia mara moja mawaidha wanayoshenezwa na viongozi wao.

Watu wa makundi haya matatu huwa hawana kosa kuwa katika hali waliyomo kwa kuwa hiyo ni hali ya kimaombile. Uhuru una maana ya kujitawala na kujitawala kuna maana ya kujihami,kujikimu,kujivalisha na kujiamlia.Endapo baa hiyo ndiyo maana ya uhuru hapana budi kundi la kwanza kujibu swali hili, “matunda wanayokawia kupeana yamepandwa na nani?“. Karima alimhuluku mwanadamu na kuupangia mastakimu yake kisha akamjalia akili, uwezo na vitu vya kumpa chakula. Maumbile nayo yakatwaa, wadhifa wa kuyabadili mazingira alimoishi mwanadamu. Hapo ughali wa maisha ukadhihirika. Kwa hivyo ikamlazimu kutumia akili na nguvu kupambana na vita vya kimaumbile ili kudumisha uhai.

Wanachukua uhuru kuwa ni hali ya kujitegemea wana mawazo sadifu sana. Uhuru huweza kuelezwa katika sehemu mbili. Kwanza ni ile hali ya mtu kujikurupusha kutoka katika nyanyaso za mtu anayetawala kwa nguvu na kumtumikisha; ikiwa sasa hana ubwana juu yake.Pili, ni kule kupewa hatamu na kuachwa pekee kumwendesha farasi usipomwendesha salama atakubwaga na kukuhasiri na mambo yatavurugika utakuwa umefuja. Tunao basi uhuru wa kimawazo na uhuru wa kiuchumi. Mawili haya hayaachani kama chungu na kia. Tukihisi kuwa tuko huru kimawazo tusiwe radhi na kuachia hapo. Hatuna budi pia kutazama upande wa uhuru wa kiuchumi.

Tulipoachiwa uamuzi wa mambo yetu wenyewe hakika tuliwekwa katika mizani kupimwa uwezo wetu wa kufanya kazi. Wajuzi wa mambo wamesema , “Uhuru ni kufanya kazi“. Bila kufanya kazi kwa bidii uhuru hukosa maana. Uhuru una maana ya kujilimia mashamba, kustawisha ufugaji,kujijengea mashule, hospitali na vyumba vizuri vya kuishi, kujifundisha kuendelea kujitolea mhanga kazini na kuikuza jamii.

Kwa kuwa viongozi ni watu wanaotegemewa sana na wale wasiojua kujiendeleza. Yabainika wanalo jukumu kubwa na gumu kuwaleta watu hao katika mkururo wa watu wengine. Walio na mawazo ya kufanyiwa kazi huku wao wataanasa, itawapasa kujiuliza mara moja,mara mbili kama wana uhuru wa kweli?

Maswali

a) Ipe taarifa hili kichwa mwafaka (Alama 1)

.....

b) Eleza kwa muhtasari maana ya uhuru. (Alama 4)

.....

.....

.....

.....

c) Kwa nini maana haieleweki kwa baadhi ya watu? (Alama 4)

.....

.....

.....

.....

d) Sisi raia tulio huru tuna wajibu gani katika taarifa? (Alama 1)

.....

.....

e) Fafanua wajibu wa viongozi katika taifa huru. (Alama 2)

.....

.....

.....

.....

f) Eleza maana ya msamiati na vifungu vifuatavyo kama yalivyotumiwa katika taarifa.

i) Kushikishwa upembo ukapambe matunda (Alama 3)

.....

ii) Kula na kusaza.

.....

iii) Huku wao wataanasa.

.....

MUHTASARI

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.

Baada ya kuchunguza kwa makini nimeshagundua kuwa wasanii maarufu huishi maisha ya kifalme. Jambo hili linadhihirika kweli ninapopiga darubini maisha yao. Mathalan,wanapoenda jamaa hawa, mashabiki hujitokeza kwa maelfu kuwalaki kuwashangilia na hata kuwatazama tu. Si ajabu kusikia sauti za watu wakisema, “Tunataka, jitokeze tafadhali tunakupenda.“

Ikiwa hushangazwi na jinsi watu wengi wanajitokeza kuwashangilia wasanii, labda utaduwaa nikikwambia kuwa baadhi ya wasanii husafiri kwa magari ya bei ghali kama vile benzi na mengio.

Usishangae pia nikikwambia kuwa baadhi yao huruka kwa ndege zao wenyewe toka mahali pamoja hadi pengine. Kila waendako jamaa hawa aghalabu huwa wamezingirwa na mameneja wanaoendesha shughuli zao, mawakala wa vyombo vya bahari pamoja na walinzi. Ama ukiona maisha ya wasanii hao, utadhani kuwa unawaona wafalme au malkia wa nchi mbalimbali.

Ikiwa hujachoshwa na hayo, pulika nikueleze mengine; kama walivyo jamaa wa aila za kifalme, picha za wasanii maarufu au "walioukata", kama tusemavyo mitaani, wana kipato kizuri kama walivyosema waliotutangulia "Mtaka cha mvunguni sharti ainame", Jamaa hawa kipato kizuri kama wameshainama kweli na sasa wanafurahia jasho lao. Jamiiya leo hulipa wasanii maarufu pesa mzo mzo. Lakini heby nikwambie kuwa fedha wanazopapta jamaa hawa si za bure: huwa wamezifanyia kazi kweli.

Usidhani kuwa pesa wanazolipwa wasanii maarufu ni zao peke yao. Pesa hizo hulipwa kodi kubwa serikalini na kodi hiyo kutumika kuendeleza huduma muhimu kwa jamii. Kwa sababu hiyo sidhani kuwa tunapaswa kuwaonea kijicho watu na vipawa vyao.
Chochote king'aacho si dhahabu. Ingawa baadhi ya wasanii wana mapesa mengi yanayowawezesha kuishi maisha ya utukufu na anasa, tusifikiri kuwa wanaishi katika pepo. Baadhi yao huzongwa na mazonge mbalimbali kama vile kutokuwa na familia imara, kupatwa na upweke wa mara kwa mara au hata wakati mwingine kufilisika. Isitoshe baadhi ya wasanii maarufu hawawezi kutoka nje ya nyumba zao au kutembea mitaani kama wewe na mimi tufanyavyo. Ama wanaweza kudhuriwa au kuhangaishwa na mashabiki wao kwa kila njia kwa sababu hiyo wasanii wengi maarufu hawafurahii maisha kama watu wa kawaida. Ingawa wanalipwa vizuri, lakini malipo hayo yana bei yake.

a) "Wasanii huishi maisha ya kifalme" Eleza jinsi kauli hii inavyodhibitishwa na taarifa.
(maneno 60- 65).
Nakala Chafu

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Nakala safi

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

b) “Chochote king’aacho si dhahabu“ Msemo huu umefafanuliwa vipi katika taarifa ? (Maneno 40 – 45)
(Alama 5)

Nakala Chafu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Nakala Safi

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

MATUMIZI YA LUGHA

a) Kwa kuzingatia jinsi ya kutamka sauti za kiswahili ni nini tofauti kati ya:

i) Irabu

.....(Alama 1)

ii) Konsonanti

..... (Alama 1)

b) Bainisha aina za nomino katika sentensi ifuatayo.

Umahiri wa kwaya ya Kwanza husababisha wanafunzi kuelewa mahubiri. (Alama 2)

.....

.....

.....

c) Andika kwa hali ya wingi;

i) Uwanja mwingineo ulichimbwa kuongezea ule wa zamani.

.....

..... (Alama 1)

ii) Asiyekujua hakuthamini

.....

..... (Alama 1)

d) Kanusha :

Nchi za Afrika mashariki zalemewa na madeni.

.....

..... (Alama 1)

e) Bainisha mifomu katika kitenzi:

Alichomolewa (Alama 3)

.....

.....

.....

f) Andika sentensi uliyopewa katika hali ya udogo wingi.

Nyumba yenyewe ilijengwa karibu na mto unaofurika mara kwa mara.

.....

.....

..... (Alama 2)

g) Tumia kirejeshi ’O’ tamati katika sentensi ifuatayo.

Myea huu ndio uliotumiwa kusuka pakacha hili.

.....

..... (Alama 1)

h) Tambulisha yambwa tendwa na yambwa tendewa katika sentensi ifuatayo.

Mwanafunzi mwenye bidii alimwandikia mwalimu majibu.

.....

.....

..... (Alama 2)

i) Andika katika usemi wa taarifa.

“Karibu Bakari, tafadhali kaa“, Maimuna alisema. “Asante, je, habari za nyumbani?“ Bakari aliuliza.

.....

.....

..... (Alama 2)

j) Tunga sentensi moja ukitumia kihusishi cha kiwango.

.....

.....

..... (Alama 1)

k). Eleza matumizi mbalimbali ya ’ni’ katika sentensi ifuatayo.

Nendeni mkamwite kanini ambaye ni mwanafunzi wangu niliyemwacha maktabani.

.....

.....

..... (Alama 2)

l) Bainisha aina ya chagizo katika sentensi hii.

Alimkimbilia adui kishujaa kabla ya kumwangamiza.

.....

.....

.....

m) Andika sentensi zifuatazo upya kwa kufuata maagizo.

i) Alicheza kwa bidii akawafurahisha wengi waliohudhuria tamasha hizo.

(Anza kwa ..... Kucheza)

.....

.....

.....(Alama 1)

ii) Karamu hiyo ilifana sana kila mtu alikula akatosheka.

(Anza kwa .....chakula)

.....

.....

..... (Alama 1)

n) Changanua sentensi ifuatayo kwa vistari.

Mgeni aliondoka jana jioni ijapokuwa wenyeji hawakumpa buriani.

.....

.....

.....

..... (Alama 4)

o) Bainisha aina ya virai katika sentensi hii.

Gari lao lilianguka kando ya jengo.

.....

.....

..... (Alama 2)

p) Tofautisha mwingiliano wa maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hii.

Ufisadi waliodhani ni <u>Siri</u> <u>ulisiri</u> na sasa wanakabiliwa na mashtaka.

.....

.....

..... (Alama 2)

q) Kamilisha jedwali

Kitenzi	Kivumishi	
Samehe	----------	
---------	Karimu	
Kakamaa	----------	(Alama 2)

r) Kwa kutunga sentensi, tofautisha vitate hivi (Alama 2)

i) Baka

.....

.....

ii) Paka.

.....

.....

s) Akifisha;

maga alipokutwa na babake akipiga simu bila idhini alishindwa kusema kwa woga akatamka ni sa me he ba baba.

.....

.....

..... (Alama 2)

t) Tunga sentensi ukitumia semi zifuatazo.

i) Piga unyende

.....

.....(Alama 1)

ii) Kusa mtu mashakani

.....

..... (Alama 1)

ISIMU JAMII

"Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu ya Bwana, kabla ya kujongea mezani pake Bwana, pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea dhambi zetu....."

a) Onyesha muktadha ambamo mazungumzo haya hutokea.

..... (Alama 1)

b) Kwa nini umechagua muktadha huo uliouchagua katika swali la (a)?

.....

.....(Alama 1)

c) Eleza sifa nne za matumizi ya lugha katika muktadha huo ambazo hazikutokeza katika mazungumzo.

(Alama 8)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....